Government of **Western Australia**
**Mental Health Commission**

Kama hutosheleza vigezo kuhitaji kuwa mgonjwa asiyekusudiwa, utaruhusiwa kuondoka.

## Una haki ya:

- kupokea maelezo kuhusu haki, kufahamishwa kabisa kuhusu matibabu yoyote yanayotoa kwako na kupata majibu kwa maswali yako
- uchunguzi wa kimwili baada ya kulazwa hospitali
- mahojiano na mtaalum wa magonjwa ya akili
- kukataa matibabu yoyote ambayo hutaki
- kuondoka hospitalini wakati wowote
- kuteua mtu aliyeteuliwa (soma brosha ya 'Mtu Aliyeteuliwa')
- kuwasiliana na watu kwa posta, simu, au baruapepe, na kutembelewa (haki hii inaweza kuwa na mipaka katika hospitali yenye mamlaka)
- ufaragha na usiri
- kufikia makumbukumbu yako ya uganga (haki hii inaweza kuzuia)
- kutunza mali yako ya kibinafsi kwa salama wakati upo hospitalini
- kutoa malalamiko kwa huduma ya afya ya akili au Ofisi ya Malalamiko ya Huduma za Afya na Ulemavu (HaDSCO) (s: 1800 813 583)
- kupata kesi yako kukaguliwa rasmi na Baraza ya Afya ya Akili (s: 08 6145 3900) kama wewe ni mgonjwa wa hiari wa muda mrefu katika hospitali yenye mamlaka.

## Maelezo zaidi

Maelezo katika brosha hii inahusisha masheria ambayo yamo Sheria ya Afya ya Akili 2014. Maelezo kuhusu Sheria hii imefupishwa katika seti ya brosha zifuatazo:

- Kupendekezwa kwenda kwa mtaalum wa magonjwa ya akili kwa uchunguzi
- Maagizo ya matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa hospitalini
- Maagizo ya matibabu ya jamii
- Maelezo kwa wagonjwa wa hiari
- Kupokea matibabu kwa ugonjwa wa akili
- Maelezo kwa watu wanaosaidia kibinafsi
- Watu walioteuliwa: Jinsi ya kuteua na maana kwake.

### Brosha zingine zinapatikana kutoka:

- Baraza ya Afya ya Akili
- Huduma ya Utetesi wa Afya ya Akili
- Kituo cha Sheria ya Afya ya Akili.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Sheria ya Afya ya Akili 2014 na nyenzo zingine, angalia tovuti ya Tume ya Afya ya Akili: www.mhc.wa.gov.au au pigia simu (08) 6272 1200

This document can be made available in other languages and alternative formats on request.

Published by the Mental Health Commission (2015)

# Maelezo kwa wagonjwa wa hiari hospitalini



Brosha hii inakupa maelezo kuhusu haki zako ni nini na unachoweza kutazamia ukipata matibabu kwa ugonjwa wa akili kama mgonjwa wa hiari hospitalini.

## Njia ya kuwa mgonjwa wa hiari hospitalini

Ukiwa umelazwa hospitalini kama mgonjwa wa hiari ni kwa sababu:

- Mtaalum wa magonjwa wa akili aliamini utapata faida kwa matibabu na utunzaji utakayopokea hospitalini, na
- Wewe (au mtu anayeweza kutoa ruhusa kwa ajili yako – kama mlezi) alikubali kwa wewe kulazwa.

## Unaweza kutazamia nini?

Wewe utakuwa mmojawapo wa namba ya wagonjwa wadini na wafanyakazi wataeleza masharti na taratibu kuhusu kukaa wadini. Wakati upo hospitalini utamwona mtaalum wa magonjwa wa akili na wafanyakazi kama wanasaikolojia, wafanyakazi wa ustawi wa jamii, wataalum wa tibu ya shughuli na muuguzi.  Utapata kadirio kamili ya kiwili na kiakili kuamua matibabu mazuri na utunzaji mzuri kwa ugonjwa wako wa akili yatakuwa nini.

## Unaweza kupata matibabu gani?

Matibabu yanaweza kuwa pamoja na madawa pamoja na tiba ya shughuli, ushauri nasaha wa mtu mmoja au wa kundi, miradi ya kisaikolojia na tiba ya mtukutiko wa umeme.

Kuwa mgonjwa wa hiari kuna maana yake kwamba matibabu yoyote hayawezi kupewa kwako bila ruhusa inayofahamishwa kutoka wewe mwenyewe (au mtu anayeweza kutoa ruhusa kwa ajili yako – kama mlezi).

Ili unaweza kutoa ruhusa inayofahamishwa lazima unaweza:

- Kuelewa maelezo kuhusu matibabu yako, ufafanuzi kuhusu matibabu mengine na onyo ya hatari zozote,
- Kuelewa mambo yanayohusu uamuzi wako wa matibabu,
- Kuelewa matokeo ya uamuzi wako wa matibabu,
- Fikiria kwa makini vipengele vinavyohusu uamuzi wako, na
- wasiliana uamuzi wako.

Lazima pia upewe muda wa kutosha kufikiria maelezo hayo, uliza maswali na omba maelezo au ushauri zaidi.

Ukikataa matibabu na wafanyakazi wanaona matibabu ni lazima kuokoa maisha yako au kukuzuia kusababisha madhara ya kiakili kwako au kwa wengine, ndipo matibabu yanaweza kupewa bila ruhusa. Hii inaitwa matibabu ya dharura ya magonjwa ya akili.

## Kuruhusu na kuondoka hospitalini

Kama mgonjwa wa hiari unaweza kuondoka hospitalini wakati wowote unaotaka, au mtaalum wako wa magonjwa wa akili anaweza kukuruhusu. Ukiwa unafikiri kuhusu kujiruhusu ni muhimu kwamba uizungumze kwanza na mtaalum wako wa magonjwa ya akili na wafanyakazi wengine.

## Unaweza kuzuia hospitalini kupinga nia zako?

Kama ukitaka kuondoka hospitali kupinga ushauri wa uganga na daktari au mweledi mwenye mamlaka wa afya ya akili (mweledi wa afya ya akili mwenye sifa sana) anaona kwamba unahitaji agizo la matibabu yasiyokusudiwa, yeye anaweza kukupendekeza kwa uchunguzi kwa mtaalum wa magonjwa ya akili na pendekezo la Fomu 1A.

Kama ukiwemo hospitali yenye mamlaka (yaani hospitali inayolaza pia wagonjwa wasiokusudiwa), ndipo unaweza kuzuia kuondoka kwa muda hadi masaa 6 ili daktari/mweledi anaweza kukuona na kuamua kwa vyovyote vile kukupendekeza kwenda mtaalum wa magonjwa wa akili.

Katika uchunguzi, mtaalum wa magonjwa wa akili, mtaalum wa magonjwa ya akili atafikiri vigezo zifuatazo, ili kuamua kwa vyovyote vile unahitaji matibabu yasiyokusudiwa:

- Una ugonjwa wa akili ambao unaohitaji matibabu?
- Kuna hatari ya maana kwako mwenyewe au kwa mtu mwengine kama hupati matibabu?
- Una afya nzuri ya kutosha kuweza kuamua uamuzi kuhusu matibabu?
- Kuna njia yenye mipaka kidogo zaidi ya kukupa matibabu badala ya matibabu yasiyokusudiwa?